# AMALI ZENYE KUFUNGUA MILANGO YA THAWABU

## أبواب الأجور - سواحيلي

Kimetafsiriwa na kuhakikiwa na:
Ally Nassor Ally
Abdallah Ally Chumbe
Abubakar Kassimu Abubakar
Yassir Salim

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
Tel: 966 164234466 - Fax: 966 164234477

بسم الله الرحمن الرحيم

## Utangulizi:

Sifa Njema zote zinamstahiki Allah, na Rehema na Amani zimshukie Mjumbe wa Allah, Ama baada ya hayo:

Ewe ndugu yangu Muislam: Dunia ni uwanja wa Mashindano na kufaulu kimalipo, tumekuwekea kwenye kijitabu hiki milango mingi ya namna ya kupata malipo ili uchume mambo mema. Tumenukuu mambo ambayo yapo sahihi kutoka kwa Mtume ziwe juu yake Rehema na Amani zilizotakasika. Zitumie juhudi zako ili upate fungu kubwa katika hayo, na kumbuka hakika msingi wa kukubaliwa matendo, na kuzidishiwa mambo mema unatokana na kumtakasia Allah – Mtukufu - matendo, na ukweli katika kumfuata Mtume wake – Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake.

Miongoni mwa upana wa Rehema za Allah na Ukubwa wa Fadhila Zake, ni pale Alipoyawekea matendo mepesi malipo makubwa. Jilazimishe ewe ndugu yangu na milango hii, na ukiweza

asikutangulie Mtu yeyote kwa Allah katikiam kheri hizi, basi fanya hivyo.

Hakika katika kukusanya katika kitabu hiki tumechagua katika Hadithi zilizoafikiwa usahihi wake na Imamu Bukhari na Muslim kwa matamshi ya Bukhari, isipokuwa zile tulizoziashiria.

Tunamuomba Allah Aikubali kazi hii, na Aeneze manufaa yake, kwani hakika Yeye ni Mwenye Kulitawalia hilo na ni Mwenye Kuliweza.

# Fadhila za Qur’an Tukufu

١ – **حفظ القرآن:** عن عائشة ﵂، عن النبي ـ ﷺ ـ قال: (( مثل الذي يقرأ القرآن وهو حافظٌ له ، مع السفرة الكرام البررة ، ومثل الذي يقرأ القرآن ، وهو يتعاهده ، وهو عليه شديدٌ ، فله أجران ))
[ متفق عليه: ٤٩٣٧ ، ٧٩٨ ]

**1. Kuihifadhi Qur’an:** Kutoka Kwa Aisha ﵂ kutoka kwa Nabii ﷺ amesema: *"Mfano wa mwenye kuisoma Qur’an na akiwa ameihifadhi, yupo pamoja na malaika wema, na mfano wa anayesoma Qur’an na akiwa anagugumia na ilhali ni ngumu kwake, basi atapata malipo mara mbili."* [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 4937, 798].

٢ – **تلاوة القرآن الكريم:** عن أبي أمامة الباهلي ـ ﵁ ـ قال: سمعت رسول الله ـ ﷺ ـ يقول : (( اقرءوا القرآن ، فإنه يأتي يوم القيامة شفيعًا لأصحابه ... الحديث )) [ رواه مسلم: ٨٠٤ ]

**2. Kuisoma Qur’an tukufu:** Kutoka Abu Umama al-Baahili ﵁ amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema: *"Someni Qur’an, kwani*

*haki-ka itakujieni siku ya Qiyama ikiwa ni muombezi kwa watu wake."* [Ameipokea Muslim: 804].

٣- **تعلم القرآن وتعليمه:** عن عثمان ﷺ ، عن النبي - ﷺ - قال: ((خيركم من تعلم القرآن وعلمه ))[ رواه البخاري: ٥٠٢٧ ]

**3. Kujifunza Qur'an na kuifundisha:** Kutoka kwa Uthmani ﷺ kutoka kwa Nabii ﷺ amesema: *"Mbora wenu ni Yule aliyejifunza Qur'an na akaifundisha."* [Ameipokea Bukhari: 5027].

٤- **سورة الإخلاص:** عن أبي الدرداء ﷺ ، عن النبي - ﷺ - قال: ((أيعجز أحدكم أن يقرأ في ليلة ثُلثَ القرآن؟ )) قالوا: وكيف يقرأ ثلث القرآن؟ قال: (( قُلْ هُوَ اللهُ أَحَدٌ، تعدِلُ ثلث القرآن ))[رواه البخاري ومسلم: ٥٠١٥ ، ٨١١ ]

**4. Suratu *al-Ikhlas*:** Kutoka kwa Abuu Al-Dardaai ﷺ amesema, Mtume ﷺ amesema, *"Hivi anashindwa mmoja wenu kusoma theluthi ya Qur'an usiku mzima?"* Wakasema: 'Anasomaje Theluthi ya Qur'an?' Akasema: *"(Kusoma) Kul huwa Allahu ahad" (Sema, Allah ni Mmoja) ni sawa na Theluthi ya Qur-an."* [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 501, 811]

٥ – **المعوذتين:** عن عقبة بن عامر ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: ((ألم تر آيات أُنزلت الليلة لم يُرَ مِثلُهن قط ؟: ﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الفَلَقِ ﴾ و ﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴾ )) [ رواه مسلم:٨١٤ ]

**5. Sura mbili za kinga**: Kutoka kwa Uqbah bin Aamir رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Nikwambie ayah zilizoshushwa usiku haijapata kuonekana mfano wake kabisa? "Kul a'audhu birabil Falaqi ''Sema ninajilinda kwa Mola Mlezi wa mapambazuko" (Asubuhi) na "Kul a'audhu birabbil nnasi (Sema ninajilinda kwa Mola wa watu)."* [Ameipokea Muslim: 814].

٦ – **سورة البقرة:** عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله ـ ﷺ – قال : (( لا تجعلوا بيوتكم مقابر، إنَّ الشيطان ينفر من البيت الذي تُقرأ فيه سورة البقرة)) [ رواه مسلم : ٧٨٠ ]

**6. Sura *al-Baqarah:*** Kutoka kwa Abuu Hurayrah رضي الله عنه Hakika Mtume ﷺ amesema: *"Msizifanye Nyumba zenu kuwa makaburi, Hakika Shetani anakimbia Nyumba inayosomwa Suratu Al-Baqarah ndani yake."* [Ameipokea Muslim: 780]

٧- **سورة البقرة وآل عمران:** عن أبي أمامة الباهلي ـ رضي الله عنه ـ قال: سمعت رسول الله ـ ﷺ ـ يقول: (( اقرءوا القرآن، فإنه يأتي يوم القيامة شفيعًا لأصحابه، اقرءوا الزهراوين: البقرة وسورة آل عمران، فإنهما يأتيان يوم القيامة كأنهما غمامتان، أو كأنهما غيايتان، أو كأنهما فِرقَانِ من طير صواف، تُحاجان عن أصحابهما، اقرءوا سورة البقرة، فإنَّ أخذها بركة، وتركها حسرة، ولا يستطيعها البطلة )) [رواه مسلم: ٨٠٤]

**7. Suratu *al-Baqara* na *Ali Imraan*:** Kutoka kwa Abuu Umama al-Baahily رضي الله عنه amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema: *"Isomeni Qur'-an, hakika itakuja Siku ya kiyama ikiwa ni kiombezi kwa aliyeisoma, zisomeni Al-Zahrawa-yni: al-Baqara na Al-Imran, hakika hizo zitakuja siku ya kiyama zikiwa kama mawingu ya mvua, au vivuli, au kama makundi mawili ya ndege yaliyopanga safu, yakiwa yanawatetea wale waliozisoma, Isomeni Surat al-Baqara, hakika kuisoma hiyo ni Baraka, na kuiacha hiyo ni majuto, na wala hawaiwezi hiyo Wachawi."* [Muslim: 804]

٨- **آية الكرسي:** عن أبي بن كعب ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( ... يا أبا المنذر! أتدري أيُّ آية من كتاب الله معك أعظم؟ )) قُلْتُ: ﴿ اللهُ لَا إِلَـهَ

إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴾ فضَرَبَ في صدري وقال : (( [والله] ليهنكَ العلـمُ أبـا المنذر )) [ رواه مسلم : ٨١٠ ]

**8. *Aayatu Al-Kursiy*:** Kutoka kwa Ubayy bin Ka`abi ﷛ amesema: Amesema Mtume ﷺ aliniuliza *"...Ewe Baba wa Mundhir! Hivi unajua ni Aya ipi kwenye Kitabu cha Allah ni tukufu kwako?'* Nikajibu: "*(Allahu laa ilaha illaa huuwal hayyul qayuumu)* Akanipiga kifuani na akasema: *((Wallahi ilimu ikubariki, Abu Al-Mundhir)) [Imepokewa na Muslim: 810]*

**٩ – آخر سورة البقرة:** عن أبي مسعود ـ ﷛ ـ قال: قال النبي ﷺ : (( من قرأ بالآيتين من آخر سورة البقرة في ليلة كفتاه )) [ متفق عليه: ٥٠١٠ ، ٨٠٨ ]

**9. Mwisho wa *Surat al-Baqarah*:** Kutoka kwa Abuu Masoud ﷛ amesema: Nabii ﷺ amesema, *"Mwenye kusoma Aya mbili za mwisho wa Suratul-Baqara usiku zitamtosha."* [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 5010, 808]

* Imamu Al-Nawawiy amesema: – Allah Amrehemu – "Zitamtosha kutokana na kisimamo cha usiku, Na kukasemwa kutokana na Shetani, kukasemwa kutokana na maafa, na inawezekana yakawa yote hayo."

١٠ –**حفظ أول سورة الكهف:** عن أبي الدرداء - رضي الله عنه - أنَّ النبي - صلى الله عليه وسلم - قال: ((من حَفِظَ عشر آيات من أول سورة الكهف ، عُصِمَ من الدجال )) [رواه مسلم: ٨٠٩] وفي رواية أخرى لمسلم: (( من حفظ عشر آيات من آخر سورة الكهف... الحديث ))

**10. Kuhifadhi mwanzo wa *Surat Al-Kahfi*:** Kutoka kwa Abuu Al-Dardaai رضي الله عنه Hakika Nabii صلى الله عليه وسلم amesema: *"Mwenye kuhifadhi Aya kumi za mwanzo wa Suratu Al-Kahfi, atalindwa dhidi ya shari za Masihi Dajjali."* [Ameipokea Muslim: 809]

Na katika riwaya nyengine ya Muslim: *"Mwenye kuhifadhi Aya kumi za mwisho wa Surat Al-Kahfi…"*

# Fadhila za Kumtaja Allah Mtukufu

١١ – **كثرة ذكر الله تعالى:** عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: «سبق المُفَرِّدُون» قالوا: وما المفردون؟ يا رسول الله. قال: «الذاكرون الله كثيرًا، والذاكرات» [رواه مسلم: ٢٦٧٦]

**11. Kumtaja Allah Mtukufu kwa wingi:** Kutoka kwa Abuu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, "Wameshinda wenye kujitenga." Wakauliza: 'ni kina nani hao wenye kujitenga? Ewe Mtume wa Allah.' Akasema: *'ni wanaume na wanawake wenye kumtaja Allah kwa wingi."* [Ameipokea Muslim: 2676]

١٢ – وعن أبي موسى ـ رضي الله عنه ـ قال: قال النبي الله ﷺ: «مَثَلُ الذي يذكر ربه، والذي لا يذكر ربه، مَثَلُ الحي والميت» [متفق عليه: ٦٤٠٧، ٧٧٩]

ولفظ مسلم: «مَثَلُ البيت الذي يُذكر الله فيه، والبيت الذي لا يُذكر الله فيه، مَثَلُ الحي والميت»

**12.** Kutoka kwa Abuu Mussa رضي الله عنه amesema, Nabii ﷺ amesema, *"Mfano wa mwenye kumtaja Mola wake na Yule asiyemtaja Mola wake, ni mfano*

*wa aliye hai na aliye kufa."* [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: [6407, 779]

Na kwa tamko la Muslim: *"Mfano wa Nyumba inayotajwa Allah ndani yake, na Nyumba ambayo hatajwi Allah ndani yake, ni kama mfano wa aliye hai na aliye kufa."*

١٣ – **التسبيح:** عن سعد ـ رضي الله عنه ـ قال: كنا عند رسول الله ـ ﷺ ـ فقال: ((أيعجز أحدكم أنَّ يكسب كل يوم ألف حسنة ؟ )). فسأله سائل من جلسائه: كيف يكسب أحدنا ألف حسنة ؟ قال: (( يسبح مئة تسبيحةٍ فيكتب له ألف حسنة، أو يحط عنه ألف خطيئة )) [ رواه مسلم: ٢٦٩٨ ]

**13. Kumsabihi Allah:** Kutoka kwa Sa`ad رضي الله عنه amesema: Tulikuwa na Mtume ﷺ akasema: *"Hivi anashindwa mmoja wenu kuchuma mema elfu moja kila siku?"* Akauliza mmoja wa aliyekua naye: 'Vipi mmoja wetu atachuma mema elfu moja?' Akamjibu: *"(Mtu) anamsabihi Allah mara mia moja, anaandikiwa mema elfu moja, au anasemehewa madhambi elfu moja."* [Ameipokea Muslim: 2698]

١٤- وعن أبي هريرة ﷺ ، أن رسول الله - ﷺ - قال: (( من قال : سبحان الله وبحمده في يوم مئة مرة حطت عنه خطاياه وإن كانت مثل زبد البحر)) [متفق عليه: ٦٤٠٥، ٢٦٩١ ]

**14.** Na kutoka kwa Abuu Hurayrah رضي الله عنه Hakika Mtume ﷺ amesema: *"Atakayesema (Sub`ha-na Llahi Wabihamdihi) mara mia moja kwa siku, atasamehewa madhambi yake hata yakiwa kama povu la bahari (kwa wingi wake)."* [Imeafikiwa Usahihi wake na Bukharin Muslim: 6405, 2691]

١٥- وعنه - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله ﷺ: (( من قال حين يصبح وحين يمسي: سبحان الله وبحمده ، مئة مرة لم يأتِ أحدٌ يوم القيامة بأفضل مما جاء به، إلا رجلٌ قال مثل ما قال، أو زاد عليه )) [ رواه مسلم: ٢٦٩٢ ]

**15.** Na kutoka kwake pia (Abuu Hurayrah) رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Ambaye atasema Asubuhi na jioni (Sub`ha-na Llahi Wabihamdihi) mara mia moja, hatokuja yeyote siku ya Kiyama na kitu bora zaidi kama alichokuja nacho yeye, isipokuwa Mtu atakaye-sema kama hayo au akazidisha."* [Ameipokea Muslim: 2692]

١٦- وعنه رضي الله عنه، عن النبي - ﷺ - قال: ((كلمتان خفيفتان على اللسان، ثقيلتان في الميزان ، حبيبتان إلى الرحمن: سبحان الله وبحمده ، سبحان الله العظيم )) [ متفق عليه: ٦٤٠٦ ، ٢٦٩٤ . وهذا لفظ مسلم ]

**16.** Na kutoka kwake (Abuu Hurayrah) رضي الله عنه kutoka kwa Nabii wa Allah ﷺ amesema: *"Maneno mawili mepesi katika ulimi (kutamkika), Mazito kwenye mizani, yanayo pendeza zaidi kwa Rrahman (Allah): "Sub`ha-na Llahi wabihamdihi Sub`ha-na Llahil 'Adhiim."* [Imeafi-kiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 2694, 6406. Na hili ni tamko la Muslim]

١٧ – وعنه ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( لأن أقول: سبحان الله، والحمد لله، ولا إله إلا الله ، والله أكبر ، أحب إليَّ مما طلعت عليه الشمس)) [ رواه مسلم: ٢٦٩٥ ]

**17.** Na kutoka kwake pia Abuu (Hurayrah) رضي الله عنه amesema: Mtume wa Allah ﷺ amesema, *"Mimi kutamka: (Sub'ha-na Llahi, Walhamdu li Llahi, Walaa ilaaha illa Allahu Wallahu Akbaru) Inapendeza zaidi kwangu kuliko vile vilivyo chomozewa na jua."* [Ameipokea Muslim: 3695]

١٨ – وعنه رضي الله عنه ، عن رسول الله ﷺ: (( من سبح الله في دبر كل صلاة ثلاثًا وثلاثين ، وحَمِدَ الله ثلاثًا وثلاثين ، و كَبَّرَ الله ثلاثًا وثلاثين ، فتلك تسعة وتسعون ، وقال تمام المئة : لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، له الملك

وله الحمد وهو على كل شيء قدير ، غُفِرَت خطاياه وإن كانت مثل زبد البحر)) [ رواه مسلم: ٥٩٧ ]

**18.** Na kutoka kwake pia Abuu (Hurayrah) رضي الله عنه kutoka kwa Mtume wa Allah ﷺ amesema, *"Mwenye kusema* **Sub'ha-na Allah.** *mara thelathini na tatu, akasema* **Al-hamdu lillah** *mara thelathini na tatu, na akasema* **Allahu Akbar** *mara thelathini na tatu, hizo zitakuwa tisini na tisa, na kasha akasema kwa kukamilisha mia:* **'Laa Ilaaha illa Llahu wa`hdahu laa shariika lahu, lahul Mulku walahul hamdu wahuwa 'Alaa kulli shay-in Qadiir,** *(Hapana anayepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Allah Peke Yake, hana mshirika, Ufalme ni Wake, na Sifa Njema zote ni Zake, Naye ni Muweza wa kila kitu, atasamehewa ma-dhambi yake hata kama ni mfano wa mapovu ya bahari (kwa wingi wake)."* [Ameipokea Muslim: 597]

١٩ – **لا حول ولا قوة إلا بالله:** عن أبي موسى الأشعري ـ رضي الله عنه ـ قال: قال لي رسول الله ﷺ : (( ألا أدُلك على كلمةٍ من كنز الجنة ؟ )) قلت: بلى ، قال: (( لا حول ولا قوة إلا بالله )) [ متفق عليه: ٦٤٠٩ ، ٢٧٠٤ ]

**19. Hakuna Hila wala Uwezo isipokuwa wa Allah:** Kutoka kwa Abuu Musa Al-Ash`ariy ﷺ amesema: aliniambia Mtume wa Allah ﷺ, *"Je, nisikujuze neno katika miongo-ni mwa hazina za Peponi?"* Nikasema: niambie, akase-ma: ***"Laa haula wala kuwwata illaa billah."*** *(Hakuna Hila wala uwezo isipokuwa wa Allah)* [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 6409, 2704]

**٢٠- سيد الاستغفار:** عن شداد بن أوس رضي الله عنه، عن النبي - ﷺ - قال: «سيد الاستغفار أن يقول: اللهم أنت ربي لا إله إلا أنت، خلقتني وأنا عبدك، وأنا على عهدك ووعدك ما استطعت، أعوذ بك من شر ما صنعت، أبوء لك بنعمتك عليَّ، وأبوء بذنبي، فاغفر لي، إنه لا يغفر الذنوب إلا أنت» قال: «ومن قالها من النهار موقنًا بها، فمات من يومه قبل أن يمسي، فهو من أهل الجنة، ومن قالها من الليل، وهو موقنٌ بها، فمات قبل أنْ يصبح، فهو من أهل الجنة» [رواه البخاري: ٦٣٠٦]

**20. Bwana wa Msamaha:** Kutoka kwa Shaddaad bin Ausi ﷺ Kutoka kwa Nabii wa Allah ﷺ amesema: *"Bwana wa Msamaha ni kuse-ma: Eee Allah Wewe ni Mola wangu Mlezi, hakuna anayepaswa kuabudiwa kwa haki isipoku-wa Wewe, Umeniumba na mimi ni mja Wako, na mimi*

*nipo kwenye ahadi Yako kwa kadri niwezavyo, ninajilinda Kwako kutokana na shari nilizozifanya, nakiri Neema Zako kwangu, na nakiri dhambi zangu Kwako, nisamehe hakika hasamehi Madhambi isipokuwa Wewe."* Akasema: "*Na mwenye kuisema wakati wa mchana hali yakuwa anayakini nayo, kisha akafa siku hiyo hiyo kabla ya kuchwa jua, basi yeye ni miongoni mwa watu wa Peponi. Na mwenye kuisema usiku hali yakuwa na yakini nayo, na akafa kabla ya asubuhi, yeye ni miongoni mwa watu wa Peponi."* [Ameipokea Bukhary: 6306]

٢١ – **الدعاء حين الاستيقاظ في أثناء النوم:** عن عبادة بن الصامت رضي الله عنه ، عن النبي - صلى الله عليه وسلم - قال: (( من تعارَّ من الليل فقال: لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، له الملك وله الحمد ، وهو على كل شيء قدير . الحمد لله ، وسبحان الله ، والله أكبر ، ولا حول ولا قوة إلا بالله ، ثم قال: اللهم اغفر لي ، أو دعا ، استُجيب له ، فإنْ توضأ وصلى قُبِلت صلاته )) [رواه البخاري: ١١٥٤]

**21. Dua wakati unapoamka usiku Usingizini:** Kutoka kwa Ubaada bin Swaamit رضي الله عنه kutoka kwa Nabii wa Allah ﷺ amesema: "*Mwenye kuamka usiku akasema: "**Laa Ilaha illa llahu wahdahu laa shariika lahu, lahul Mulku walahul hamdu wahuwa 'Alaa kulli shay-in***

***Qadir"** (Hapana Mola apasae kuabu-diwa kwa haki isipokuwa Allah Peke Yake hana mshirika, Ufalme ni Wake Yeye na Sifa Njema ni Zake, Naye ni Muweza wa kila kitu), "**Alhamduli llah**" (Sifa Njema zinamstahiki Allah Pekee), "**Wasubha-na llah**" (na Utakatifu ni Wake Allah), "**Wallahu Akbar**" (na Allah ni Mkubwa), "**Laa haula wala kuwwata illaa billah**" (wala hakuna hila yeyote wala nguvu isipokuwa Kwake Allah).' Kisha akasema, "Eee Allah nisamehe, au akaomba lolote jema atajibi-wa, na lau atatawadha na na akaswali basi hukubaliwa Sala yake."* [Ameipokea Bukhariy: 1154]

٢٢- **التهليل:** عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله - صلى الله عليه وسلم - قال: (( من قال: لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير، [في يوم ] مئة مرة كانت له عدل عشر رقاب ، وكُتبت له مئة حسنة ، ومُحيت عنه مئة سيئة ، وكانت له حرزًا من الشيطان يومه ذلك حتى يمسي، ولم يأت أحدٌ بأفضل مما جاء به إلا رجلٌ عمل أكثر منه )) [ متفق عليه: ٦٤٠٣، ٢٦٩١ ]

**22. Kutamka neno (*Laailaha illa Allah*):** Kutoka kwa Abuu Hurayrah رضي الله عنه hakika Mtume wa Allah ﷺ amesema: *"Mwenye kusema "**Laa Ilaha illa llahu wah'dahu laa shariika lahu,***

***lahul Mulku walahul hamdu wahuwa 'Alaa kulli shay-in Qadiir"*** *(Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Peke Yake Hana mshirika, Ufalme ni Wake Yeye na Sifa Njema ni Zake, naye ni Muweza wa kila kitu), mara mia moja kwa kila siku, atapata malipo ya kuwaacha huru watumwa kumi, na huandikiwa Mema mia moja, na husamehewa madhambi mia moja, na atakuwa na kinga ya Shetani siku yake nzima mpaka kunakuchwa, na hatokuja yeyote na jambo bora zaidi kama alilokuja nalo yeye, isipokuwa Mtu atakayefanya zaidi yake."* [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 2691 ،6403]

٢٣- وعن أبي أيوب الأنصاري - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله ﷺ: (( من قال لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، له الملك وله الحمد ، وهو على كل شيء قدير ، عشر مرار ، كان كمن أعتق أربعة أنفس من ولد إسماعيل ))

[ رواه مسلم: ٢٦٩٣]

**23. Kutoka kwa Abuu Ayoub al-Answaary** رضي الله عنه **amesema:** Mtume wa Allah ﷺ, *"Mwenye kusema* ***(Laa Ilaha illa llahu wah'dahu laa shariika lahu, lahul Mulku walahul hamdu wahuwa 'Alaa kulli shay-in Qadiir)****, mara kumi*

*kwa siku, malipo yake yatakuwa kama aliyewaacha huru watu wanne miongoni mwa Mtoto wa Nabii Ismail."* [Ameipokea Muslim: 2693]

٢٤_ **فضل مجالس الذكر:** عن أبي هريرة، وأبي سعيد الخدري رضي الله عنهما ، عن النبي - ﷺ - قال: (( لا يقعد قوم يذكرون الله - عز وجل - إلا حفتهم الملائكة، وغشيتهم الرحمة ، ونزلت عليهم السكينة ، وذكرهم الله فيمن عنده )) [رواه مسلم: ٢٧٠٠]

**24. Ubora wa Vikao vya Kumtaja Allah:** Kutoka kwa Abuu Hurayrah na Abuu Said Al-Khudriy رضي الله عنهما kutoka kwa Nabii ﷺ amesema: *"Hawatakaa watu wakimtaja Allah - Mtukufu - isipokuwa huzungukwa na Malaika, hufunikwa na Rehema za Allah, na watashuki-wa na utulivu na Allah Atawataja vizuri kwa walio kuwa mbele yake (malaika)."* [Muslim: 2700]

٢٥- **الصلاة على النبي ﷺ:** عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله - ﷺ - قال: ((من صلى عليَّ واحدةً ، صلى الله عليه عشرًا )) [رواه مسلم: ٤٠٨]

**25. Kumswalia Mtume ﷺ:** Kutoka kwa Abuu Hurayrah رضي الله عنه hakika Mtume wa Allah ﷺ amesema: *"Mwenye kuniswalia Mara moja,*

*Allah Atamrehemu mara kumi."* [Ameipokea Muslim: 408]

٢٦- **حمد الله بعد الأكل والشرب:** عن أنس بن مالك ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( إن الله ليرضى عن العبد أن يأ كل الأكلة فيحمده عليها ، أو يشرب الشربة فيحمده عليها )) [ رواه مسلم: ٢٧٣٤ ]

**26. Kumshukuru Allah baada ya kula na kunywa:** Kutoka kwa Anas bin Maalik رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Hakika ya Allah Anamridhia mja anayekula chakula kisha akamshukuru, au akanywa kinywaji kisha akamshukuru."* [Muslim: 2734].

# Fadhila za Udhu na Swala

٢٧ – **إحسان الوضوء:** عن عثمان بن عفان ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: ((من توضأ فأحسن الوضوء خرجت خطاياه من جسده، حتى تخرج من تحت أظفاره)) [ رواه مسلم: ٢٤٥ ]

**27. Kutawadha vizuri:** Kutoka kwa Uthmani bin Affani رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, "*Yeyote mwenye kutawadha, akaufanya vizuri udhu, yanatoka Madhambi yake kutoka mwilini mwake, mpaka yanatokea chini ya kucha zake."* [Amepokea Muslim: 245]

٢٨– وعنه ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ : (( من أتم الوضوء كما أمر الله تعالى ، فالصلوات المكتوبات كفارات لما بينهن )) [ رواه مسلم: ٢٣١ ]

**28.** Imepokewa kwake (Uthmani) رضي الله عنه amese-ma: Mtume ﷺ amesema, "*Mwenye kuutimiza Udhu (Kutawadha) kama Alivyoamrisha Allah - Mtukufu- basi Swala za Faradhi zote zinakuwa ni kafara ya (madhambi) yaliyo kuwa kati ya swala hizo."* [Amepokea Muslim: 231]

٢٩ - **التشهد بعد الوضوء:** عن عمر بن الخطاب ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( ما منكم من أحد يتوضأ، فيسبغ الوضوء ثم يقول: أشهد أن لا إله إلا الله، وأنَّ محمدًا عبده ورسوله، إلاَّ فتحت له أبواب الجنة الثمانية، يدخل من أيها شاء )) [رواه مسلم: ٢٣٤]

**29. Shahada baada ya Udhu**: Kutoka kwa Umar Bin al-Khatwabi رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Hapanapo mmoja wenu akatawa-dha, na akaufanya vizuri udhu wake, kisha akase-ma: "Nashuhudia hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na hakika Muhammad ni mja wake na mjumbe wake, ila itafunguliwa kwake milango ya pepo minane, aingie autakao."* [Ameipokea Muslim: 234]

٣٠- **الترديد مع المؤذن ثم الصلاة على النبي ﷺ:** عن عبدالله بن عمرو رضي الله عنهما، أنه سمع النبي ـ ﷺ ـ يقول: (( إذا سمعتم المؤذن فقولوا مثل ما يقول، ثم صلوا عليَّ، فإنه من صلى عليَّ صلاة، صلى الله عليه بها عشرًا ... الحديث)) [رواه مسلم: ٣٨٤]

**30. Kumfatisha anayeadhini kisha kumswa-lia Mtume ﷺ:** Kutoka kwa Abdallah bin Amru – رضي الله عنهما yeye alimsikia Nabii ﷺ akisema: *"Mukim-sikia mwenye kuadhini, basi nanyi semeni kama*

*anavyosema yeye, kisha niswalieni, hakika atakayeniswalia mara moja, Allah Atamrehemu mara kumi...".* [Amepokea Muslim: 384]

٣١- **الدعاء حين سماع المؤذن:** عن جابر بن عبدالله رضي الله عنه ، أن النبي - صلى الله عليه وسلم - قال: (( من قال حين يسمع النداء: اللهم رب هذه الدعوة التامة والصلاة القائمة، آتِ محمدًا الوسيلة والفضيلة، وابعثه مقامًا محمودًا الذي وعدته ؛ حَلَّت له شفاعتي يوم القيامة )) [ رواه البخاري: ٦١٤]

**31. Dua baada ya kusikia Adhana:** Kutoka kwa Jabir bin Abdillah رضي الله عنه kwamba Mtume صلى الله عليه وسلم amesema: *"Mwenye kusema anaposikia mwito (Adhana): Eee Mola Mlezi wa wito huu mkamilifu na Swala iliyothibiti, mpe Muhammad daraja ya juu peponi, na fadhila, na Umnyanyue kwenye nafasi iliyotukuka Uliyomuahidi" isipokuwa uombezi wangu utatolewa kwake Siku ya Kiyama."* [Imepokewa na Al-Bukhari: 614].

٣٢- **فضل الأذان:** عن أبي سعيد الخدري - رضي الله عنه - قال: سمعت رسول الله - صلى الله عليه وسلم - يقول : (( لا يسمع مدى صوت المؤذن جنٌ ولا إنسٌ ، ولا شيءٌ إلا شهد له يوم القيامة ))[ رواه البخاري: ٦٠٩ ]

**32. Fadhila ya Adhana:** kutoka kwa Abii Saiid al-Khudry رضي الله عنه amesema: Nimemsikia Mtume

ﷺ akisema: *"Haisikii sauti ya Muadhini Jini, Binadamu, wala chochote kile, isipokuwa kitakuja kumtolea ushuhuda siku ya Kiyama."* [Amepokea Bukhary: 609].

٣٣- **بناء المساجد:** عن بكير عن عثمان بن عفان - رضي الله عنه - قال عند قول الناس فيه حين بنى مسجد الرسول ﷺ : ( إنكم أكثرتم ، وإني سمعت النبي - ﷺ - يقول: (( من بنى مسجدًا - قال بُكير: حسبت أنه قال: يبتغي به وجه الله - بنى الله له مثله في الجنة )) [متفق عليه: ٤٥٠ ، ٥٣٣]

**33. Kujenga Misikiti:** Kutoka kwa Bukayr, kutoka kwa Uthmani Bin Affani رضي الله عنه alisema, pale waliposema watu wakati yeye alipotaka kuujenga Msikiti wa Mtume ﷺ amesema, "Hakika ninyi mmezidisha maneno, mimi nilimsikia Nabii ﷺ akisema: *'Mwenye kujenga Msikiti."* Akasema Bukayr: Nadhania kuwa alisema: *'Anatafuta Radhi za Allah, basi Allah Atamjengea Nyumba mfano wake pepo-ni."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 450,533]

٣٤- **التأمين مع الإمام:** عن أبي هريرة - رضي الله عنه - أن رسول الله - ﷺ - قال: ((إذا أمَّن الإمامُ فأمنوا ، فإنهُ من وافقَ تأمينُه تأمينَ الملائكةِ ، غُفر لهُ ما تقدم من ذنبه )) [ متفق عليه: ٧٨٠ ، ٤١٠ ]

**34. Kuitikia Amiin pamoja na Imam:** Kutoka kwa Abuu Hurayra ﵁ hakika Mtume ﷺ amesema: *"Atakapoitikia Imam Aamiin, nanyi mseme Aamiin, hakika mwenye kuafiki (kuwa sawa) Amiin yake pamoja na Amiin ya Malaika, atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 780,410]

٣٥- **التبكير إلى الصلاة :** عن أبي هريرة ـ ﵁ ـ قال: قال رسول الله ﷺ : (( ... ولو يعلمون ما في التهجير لاستبقوا إليه ... الحديث ))

[متفق عليه: ٦١٥، ٤٣٧ ]

**35. Kuwahi Swala mapema:** kutoka kwa Abuu Hurayra ﵁ amesema: ﷺ amesema, *"...na laiti wangejua (malipo ya) kuwahi mapema, basi wangeshindana kuwahi (kufika)..."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 615,437]

٣٦- **التطهر في المنزل ثم المشي إلى المسجد :** عن أبي هريرة ـ ﵁ ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( من تطهر في بيته ثم مشى إلى بيت من بيوت الله ، ليقضي فريضة من فرائض الله ، كانت خطواته إحداهما تَحُطُّ خطيئة ، والأخرى ترفع درجة )) [ رواه مسلم: ٦٦٦ ]

**36. Kujitwaharisha nyumbani kisha kwenda Msikitini:** Kutoka kwa Abuu Hurayra ﵁ amesema: ﷺ amesema, *"Mwenye kujitwaharisha nyumbani kwake, kisha akaenda kwenye nyumba miongoni mwa nyumba za Allah, ili atekeleze Faradhi moja miongoni mwa Faradhi za Allah, zinakuwa hatua zake, moja inafuta madhambi na nyingine inanyanyua daraja."* [Amepokea Muslim: 666]

٣٧- **كثرة الخطا إلى المساجد :** عن أبي هريرة ﵁ ، أن رسول الله ـ ﷺ ـ قال: (( ألا أدلكم على ما يمحو الله به الخطايا ، ويرفع به الدرجات )) قالوا: بلى يا رسول الله ، قال: (( إسباغ الوضوء على المكاره ، وكثرة الخطا إلى المساجد ، وانتظار الصلاة بعد الصلاة، فذلكم الرباط )) [ رواه مسلم: ٢٥١ ]

**37. Hatua nyingi kwenda Misikitini:** Kutoka kwa Abuu Hurayra ﵁ hakika Mtume ﷺ amesema: "Je! Nisikuambieni kwa njia gani Allah Hufuta madhambi na Kunyanyua daraja?" Wakasema: 'Tuambie, Ewe Mtume wa Allah.' Akasema: *"Kutawadha wakati wa ugumu, na hatua nyingi za kwenda Misikitini, na kungojea Swala baada ya Swala, hiyo ndiyo Ribat, (kujizuia kuliko bora zaidi)."* [Amepokea Muslim: 251]

٣٨- وعنه رضي الله عنه، عن النبي - ﷺ - قال:((من غدا إلى المسجد أو راح، أعد الله له في الجنة نزلاً،كلما غدا أو راح )) [ متفق عليه: ٦٦٢ ، ٦٦٩ . وهذا لفظ مسلم ]

**38.** Na pia inapokewa kutoka kwake (Abuu Hurayra), kutoka kwa Nabii wa Allah ﷺ amesema: *"Mwenye kwenda msikitini (wakati wa asubuhi) au kwenda msikitini (wakati wa jioni) Allah Amemuandalia makazi yake peponi, kila anapokwenda wakati wa asubuhi, au anapokwenda wakati wa jioni."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 662,669. Hili ni tamko la Imam Muslim]

** Na haya makazi ni dhifa na takrima maalum kwake.

٣٩- **المحافظة على السنن الرواتب :** عن أم حبيبة - رضي الله عنها - أنها سمعت رسول الله - ﷺ - يقول:(( ما من عبد مسلم يصلي لله كل يوم ثنتي عشرة ركعة تطوعًا غير الفريضة ، إلا بنى الله له بيتًا في الجنة )) [ رواه مسلم: ٧٢٨ ]

**39. Kudumisha Sunna za *Rawatib* (Kabla na baada ya Swala ya Faradhi):** Kutoka kwa Ummi Habiba رضي الله عنها hakika yeye alimsikia Mtume ﷺ akisema: *"Hakuna mja yeyote Muislam, anaswali kwa ajili ya Allah kwa siku rakaa kumi na mbili za Sunna, sio za Faradhi, isipokuwa Allah Atamjengea nyumba peponi."* [Amepokea Muslim: 728]

٤٠ – **قيام الليل :** عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله - صلى الله عليه وسلم - سُئل : أيُّ الصلاة أفضل بعد المكتوبة، فقال: (( أفضل الصلاة بعد الصلاة المكتوبة: الصلاة في جوف الليل ))[ رواه مسلم: ١١٦٣ ]

**40. Kisimamo cha usiku:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه hakika Mtume ﷺ aliulizwa: 'Ni ipi Swala bora baada ya (sala ya) Faradhi?' Akasema: *'Swala bora baada ya swala ya Faradhi ni Swala (inayoswaliwa) kati kati ya usiku."* [Amepokea Muslim: 1163]

٤١ – **صلاة العشاء والصبح في جماعة:** عن عثمان بن عفان - رضي الله عنه - قال: سمعت رسول الله - ﷺ - يقول: (( من صلى العشاء في جماعة فكأنما قام نصف الليل ، ومن صلى الصبح في جماعة فكأنما صلى الليل كله )) [ رواه مسلم: ٦٥٦]

**41. Kuswali Jamaa, Ishaa na Al-fajiri:** Kutoka kwa Athumani Bin Afani رضي الله عنه amesema: nimemsikia Mtume ﷺ akisema: *"Mwenye kuswali Ishaa kwa Jamaa ni kama amesimama nusu ya usiku, na anayeswali al-Fajiri kwa Jamaa ni kama aliyeswali usiku wote."* [Amepokea Muslim: 656].

٤٢ – **حضور الجمعة بإحسان وضوء، واستماع، وإنصات**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( من توضأ فأحسن الوضوء، ثم أتى الجمعة فاستمع وأنصت، غُفر له ما بينه وبين الجمعة، و زيادة ثلاثة أيام ...الحديث)) [ رواه مسلم: ٨٥٧ ]

**42. Kuhudhuria Swala ya Ijumaa, akiwa ametawadha vizuri kusikiliza Khutba na kunyamaza:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, "*Mwenye kutawa-dha na akaufanya vizuri udhu wake, kisha akaenda Ijumaa, akasikiliza na akanyamaza, atasamehewa dhambi zilizopo kati ya Ijumaa na Ijumaa, na nyongeza ya siku tatu...*" [Amepokea Muslim: 857] *Sababu ya kuongezewa siku tatu, ni kwa sababu jema moja linalipwa kwa kumi mfano wake.

٤٣ – **التبكير إلى صلاة الجمعة**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( إذا كان يوم الجمعة ، وقفت الملائكة على باب المسجد ، يكتبون الأول فالأول ، ومثل المُهَجِّر ( **أي: المبكر**) كمثل الذي يهدي بدنة ، ثم كالذي يهدي بقرة ، ثم كبشاً ، ثم دجاجة، ثم بيضة ، فإذا خرج الإمام طَوَوْا صحفهم ، ويستمعون الذكر )) [ متفق عليه: ٩٢٩ ، ٨٥٠ ]

**43. Kuwahi mapema katika Swala ya Ijumaa:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema:

Mtume ﷺ amesema, "*Itakapokuwa siku ya Ijumaa, wanasimama Malaika kwenye Mlango wa Msikiti, wanaandika wa kwanza na anayefuata, na mfano kwa aliyewahi mapema ni kama mtu aliyetoa sadaka ya Ngamia, kisha (anayefuata) kama aliyetoa sadaka ya Ng'o-mbe, kisha (sadaka ya) Kondoo, kisha (sadaka ya) Kuku, kisha (sadaka ya) Yai, akitoka Imam, wanakunja nyaraka zao na wanasikiliza Dhikri."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 929, 850]

٤٤ – **الصلاة على الجنازة وشهود دفنها**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( من شهد الجنازة حتى يصلى عليها فله قيراط ، ومن شهدها حتى تدفن فله قيراطان )) قيل: وما القيراطان؟ قال: (( مثل الجبلين العظيمين )) [ متفق عليه: ١٣٢٥ ، ٩٤٥ . وهذا لفظ مسلم ]

**44. Kuswalia maiti na kushuhudia mazishi yake:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema: "*Mwenye ku-shuhudia Jeneza mpaka likaswaliwa, atapata Qirati moja, na mwenye kushuhudia mpaka akazikwa atapata Qirati mbili*.' Pakasemwa: 'Qirati mbili ni nini?' Akasema: *'ni mfano wa milima miwili mikubwa.'* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 1325,945, na hili ni tamko la Muslim]

# Fadhila za Swaumu

٤٥ – **صيام رمضان إيمانًا واحتسابًا**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( من صام رمضان إيمانًا واحتسابًا ، غُفر له ما تقدم من ذنبه )) [متفق عليه: ٣٨ ، ٧٦٠]

**45. Kufunga Ramadhani kwa kumuamini Allah na Kutaraji malipo kwake**: Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kufunga Ramadhani, kwa kumuamini Allah, na kutaraji malipo mema kutoka Kwake, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 38,760]

٤٦ – **قيام رمضان إيمانًا واحتسابًا**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: (( من قام رمضان إيمانًا واحتسابًا ، غُفر له ما تقدم من ذنبه )) [متفق عليه: ٢٠٠٩ ، ٧٥٩]

**46. Kusimama (usiku wa) Ramadhani kwa kumuamini Allah na kutaraji malipo kwake:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kusimama (usiku wa) Ramadhani, kwa*

*kumuamini Allah, na kutaraji malipo mema kwake, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia".* [Imeafikiwa usahi-hi wake na Imam Bukhari na Muslim: 2009, 759]

٤٧ – **صوم ستة أيام من شوال**: عن أبي أيوب الأنصاري ﵁ ، أن رسول الله ـ ﷺ ـ قال: (( من صام رمضان ، ثم أتبعه ستًا من شوال،كان كصيام الدهر )) [ رواه مسلم: ١١٦٤ ]

**47. Kufunga siku sita za *Shawwal* (Mfungo mosi):** Kutoka kwa Abuu Ayubu al-Answary ﵁ hakika Mtume ﷺ amesema: *"Mwenye kufunga Ramadhani, kisha akafatishia (kufunga) siku sita za Mfungo mosi, atakuwa kama amefunga Mwaka mzima."* [Amepokea Muslim: 1164]

٤٨ – **صوم ثلاثة أيام من كل شهر**: عن أبي هريرة ـ ﵁ ـ قال: (( أوصاني خليلي بثلاث ، لا أدعهن حتى أموت: صوم ثلاثة أيام من كل شهر ، وصلاة الضحى، ونوم على وتر )) [ متفق عليه: ١١٧٨، ٧٢١ ]

**48- Kufunga siku tatu kila mwezi:** Kutoka kwa Abuu Hurayra ﵁ amesema: "*Ameniu-sia kipenzi changu, mambo matatu, nisiyaache mpaka kufa: Kufunga siku tatu kila mwezi,*

*Swala ya Dhuhaa, na Kulala baada ya kusali Sala ya Witri."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 1178, 721]

٤٩ – **صوم يوم عرفة**: عن أبي قتادة ﷺ، أن رسول الله - ﷺ – قال: ((صيام يوم عرفة ، أحتسب على الله أن يكفر السنة التي قبله، والسنة التي بعده )) [ رواه مسلم: ١١٦٢ ]

**49. Kufunga siku ya Arafa:** Kutoka kwa Abuu Qatada  hakika Mtume ﷺ amesema, *"Kufunga siku ya Arafa, nataraji kwa Allah itafuta madhambi ya mwaka uliopita na mwaka unaokuja."* [Amepokea Muslim: 1162]

٥٠ – **صوم يوم عاشوراء**: عن أبي قتادة - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله ﷺ: ((صيام يوم عاشوراء ، أحتسب على الله أن يكفر السنة التي قبله)) [رواه مسلم: ١١٦٢ ]

**50. Kufunga siku ya Aashuraa:** Kutoka kwa Abuu Qatada  amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Funga ya siku ya Aashuraa, nataraji kwa Allah itafuta madhambi ya mwaka uliopita."* [Amepokea Muslim: 1162]

# Fadhila Mbali Mbali

٥١ – **التوبة** : عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ : (( من تابَ قبل أن تطلُعَ الشمسُ من مغربها ، تاب الله عليه )) [ رواه مسلم:٢٧٠٣ ]

**51. Toba (Kutubia):** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kutubia kabla ya Jua kuchomoza Maghribi, Allah Atamkubalia toba yake."* [Amepokea Muslim: 7203]

٥٢ – **فضل الحج والعمرة:** عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله ـ ﷺ ـ قال : ((العمرة إلى العمرة كفارة لما بينهما ، والحج المبرور ليس له جزاء إلا الجنة ))

[ متفق عليه: ١٧٧٣ ، ١٣٤٩ ]

**52. Fadhila ya Hijja na Umra**: Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه hakika Mtume ﷺ amesema: *"Umra mpaka Umra nyingine ni kafara (kifutio) kwa madhambi yaliyopo kati ya hizo, na Hijja iliyofanywa kwa Ikhlas (kwa ajili ya Allah), haina malipo isipokuwa pepo."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 1773, 1349]

٥٣ – **الإكثار من الأعمال الصالحة في عشر ذي الحجة**: عن ابن عباس رضي الله عنه، عن النبي - صلى الله عليه وسلم - قال: (( ما العمل في أيام أفضل منها في هذه ( **يعني أيام العشر**) )) قالوا: ولا الجهاد؟ قال: (( ولا الجهاد، إلا رجل خرج يخاطر بنفسه وماله فلم يرجع بشيء )) [رواه البخاري: ٩٦٩]

**53. Kutenda mema kwa wingi, Siku kumi za Mfungo tatu:** Kutoka kwa Ibn Abbasi رضي الله عنه kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وسلم amesema: *"Hakuna matendo kwenye siku bora zaidi kuliko siku hizi (anakusudia siku kumi).' Wakasema:* 'Hata Jihadi?' *Akasema: 'Hata Jihadi, isipokuwa mtu aliyetoka akaitia hatarini nafsi yake, na mali yake, kisha hakurudi na chochote."* [Amepokea Bukhary: 969]

٥٤ – **طلب العلم**: عن أبي هريرة - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: (( ... ومن سلك طريقًا يلتمس فيه علمًا سهل الله له به طريقًا إلى الجنة ... الحديث )) [رواه مسلم: ٢٦٩٩]

**54. Kutafuta Elimu:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume صلى الله عليه وسلم amesema, *"... na atakayepita njia akawa anatafuta elimu, Allah Atamfanyia wepesi njia ya kwenda peponi..."* [Amepokea Muslim: 2699].

٥٥ – **التفقه في الدين**: عن معاوية ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ :
((من يرد الله به خيرًا يُفَقهه في الدين )) [ متفق عليه: ٧١، ١٠٣٧]

**55- Kujifunza Dini:** Kutoka kwa Muaawiya رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, "*Yeyote ambae Allah Atamtakia kheri, Atampa ufahamu wa Dini."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 1773, 1349]

٥٦ – **الدعوة إلى الله**: عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله ـ ﷺ ـ قال : (( من دعا إلى هدى ، كان له من الأجر مثل أجور من تبعه ، لا ينقص ذلك من أجورهم شيئًا ... الحديث )) [ رواه مسلم: ٢٦٧٤ ]

**56. Kuwalingania watu kwa Allah:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, "*Mwenye kulingania jambo la uongofu, atapata malipo, mfano wa malipo ya watu waliomfuata, halipunguzi hilo kwenye malipo yao chochote kile..."* [Amepokea Muslim: 2674].

٥٧ – **الأمر بالمعروف والنهي عن المنكر**: عن أبي سعيد ـ رضي الله عنه ـ قال: سمعت رسول الله ـ ﷺ ـ يقول : (( من رأى منكم منكرًا فليغيره بيده، فإن لم يستطع فبلسانه ، فإن لم يستطع فبقلبه وذلك أضعف الإيمان )) [ رواه مسلم: ٤٩ ]

**57. Kuamrisha mema na kukataza maovu:** Kutoka kwa Abuu Said ﷺ amesema: nimemsikia Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kuona jambo ovu, basi na alibadilishe kwa Mkono wake, asipoweza basi na atumie ulimi wake, na asipoweza basi atumie Moyo wake (achukie), na hiyo ni imani dhaifu."* [Amepokea Muslim: 49]

٥٨ – **إفشاء السلام**: عن عبدالله بن عمرو رضي الله عنهما ، أنَّ رجلاً سأل النبي ﷺ: أي الإسلام خير؟ قال: (( تُطعم الطعام ، وتقرأ السلام ، على من عرفت ومن لم تعرف )) [ متفق عليه: ٦٢٣٦، ٣٩ ]

**58. Kusalimiana**: Kutoka kwa Abdallah Bin Amru رضي الله عنهما Hakika mtu mmoja alimuuliza Mtume ﷺ, "Upi Uislam bora? Akamjibu: *"Kulisha chakula, kuwatolea salam wale unao wafahamu na usio wafahamu."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 6236, 39]

٥٩ – **الحب في الله** : عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ: ((إن الله يقول يوم القيامة : أين المتحابون بجلالي ، اليوم أظلهم في ظلي، يوم لا ظل إلا ظلي )) [ رواه مسلم: ٢٥٦٦ ]

**59. Kupenda kwa ajili ya Allah:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ

amesema, *"Hakika Allah Atasema siku ya Kiyama: 'Wako wapi wanaopendana kwa ajili ya Utukufu Wangu, leo hii Niwafunike kwa Kivuli Changu, siku ambayo haina kivuli isipokuwa Kivuli Changu."* [Amepokea Muslim: 2566]

٦٠- **الصدق**: عن عبدالله - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله ﷺ: (( عليكم بالصدق، فإن الصدق يهدي إلى البر ، وإن البر يهدي إلى الجنة ، وما يزال الرجل يصدق ويتحرى الصدق حتى يكتب عند الله صديقًا ... الحديث ))

[ متفق عليه: ٦٠٩٤ ، ٢٦٠٧ . وهذا لفظ مسلم ]

**60. Kusema ukweli:** Kutoka kwa Abdallah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Jilazimisheni kuwa wakweli, hakika ukweli unapelekea katika wema, na hakika wema unapelekea mtu kuingia peponi, na ataendelea mtu kusema kweli, na atapupia ukweli mpaka ataandikwa mbele ya Allah kuwa ni mkweli..."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 6094, 2607, na hili ni tamko la Muslim]

٦١- **حسن الخلق**: عن عبدالله بن عمرو رضي الله عنهما ، أن رسول الله - ﷺ - كان يقول: (( إن من خياركم أحسنكم أخلاقًا )) [ متفق عليه: ٣٥٥٩ ، ٢٣٢١ ]

**61. Tabia njema:** kutoka kwa Abdallah Bin Amri رضي الله عنهما hakika Mtume ﷺ amesema, *"Hakika mbora*

*wenu ni yule mwenye tabia nzuri miongoni mwenu."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 3559, 2321]

٦٢ – **طلاقة الوجه**: عن أبي ذر ـ رضي الله عنه ـ قال: قال لي النبي ﷺ: (( لا تحقرن من المعروف شيئًا ، ولو أن تلقى أخاك بوجه طلق )) [رواه مسلم:٢٦٢٦]

**62. Bashasha ya uso:** Kutoka kwa Abuu Dharri رضي الله عنه amesema: aliniambia Mtume ﷺ, *"Usidharau chochote miongoni mwa mambo mema, japo kukutana na ndugu yako kwa uso wenye Bashasha (Tabasamu)".* [Amepokea Muslim: 2626]

٦٣ – **عيادة المريض**: عن ثوبان ، مولى رسول الله ﷺ ، عن رسول الله ـ ﷺ ـ قال: (( من عاد مريضًا ، لم يزل في خُرفَة الجنة )) قيل : يا رسول الله، وما خُرفة الجنة؟ قال: (( جناها )) [رواه مسلم:٢٥٦٨]

**63. Kumtembelea Mgonjwa:** Kutoka kwa Thaubaan Mtumwa wa Mtume wa Allah ﷺ - kutoka kwa Mtume ﷺ amesema, *"Yeyote mwenye kumtembelea mgonjwa, hatoacha kuwa Khurfatal-janna (mwenye kuchuma matunda ya peponi).'* Wakamuuliza, 'nini maana ya *Khur-*

*fatal-janna*?' Akasema: *'ni matunda ya peponi."* [Amepokea Muslim: 2568]

٦٤- **الرفق**: عن جرير رضي الله عنه ، عن النبي - صلى الله عليه وسلم - قال: (( من يُحرم الرفق ، يُحرم الخير)) [ رواه مسلم: ٢٥٩٢ ]

**64. Upole:** Kutoka kwa Jariyr رضي الله عنه amesem-a: Mtume ﷺ amesema, *"Atakayenyimwa upole, basi amenyimwa kheri."* [Amepokea Muslim: 2592]

٦٥- **الصبر**: عن أبي سعيد وأبي هريرة رضي الله عنهما ، أن رسول الله - صلى الله عليه وسلم - قال: ((ما يُصيبُ المسلمَ من نصبٍ ولا وصبٍ ولا همٍ ولا حَزَنٍ ، ولا أذىً ، ولا غمٍ حتى - الشوكة يشاكها - إلا كَفَّر الله بها من خطاياه )) [ متفق عليه: ٥٦٤١ ، ٢٥٧٣ ]

**65. Subira:** Kutoka kwa Abuu Said na Abuu Hurayra رضي الله عنهما Hakika Mtume ﷺ amesema, *"Haimpati Muislam tabu, wala maradhi, wala huzuni, wala maudhi, mpaka miba inayomcho-ma, isipokuwa Allah anamfutia ma-dhambi yake."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 5641, 2573]

٦٦- **كفالة اليتيم**: عن سهل بن سعد رضي الله عنه ، عن النبي - صلى الله عليه وسلم - قال: (( أنا وكافل اليتيم في الجنة هكذا )) وقال بإصبعيه السبابة والوسطى. [ رواه البخاري: ٦٠٠٥ ]

**66. Kulea mtoto yatima:** Kutoka kwa Sahli Bin Saad رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema, *"Mimi na mwenye kumlea mtoto yatima, tutakuwa peponi kama hivi."* Akawa anaashiria kwa vidole vyake viwili cha Shahada na cha kati. [Amepokea Bukhary: 6005]

٦٧- **تنفيس الكَرْب**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال النبي ﷺ : (( من نَفَّس عن مؤمن كربة من كرب الدنيا ، نَفَّس الله عنه كربة من كرب يوم القيامة ، ومن يَسَّرَ على مُعسِرٍ ، يسَّر الله عليه في الدنيا والآخرة ... الحديث ))[ رواه مسلم: ٢٦٩٩ ]

**67. Kutatua shida za watu:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kumtatulia muumini shida moja tu katika shida za Duniani, Allah atamtatulia shida moja katika shida za Siku ya Kiyama, na atakaye mfanyia wepesi mwenye uzito, Allah atamfanyia wepesi Duniani na Akhera..."* [Amepokea Muslim: 2699]

٦٨-وعن أبي قتادة ـ رضي الله عنه ـ قال: سمعت رسول الله ـ ﷺ ـ يقول: (( من سَرَه أن يُنْجِيَهُ الله من كُرَب يوم القيامة فليُنَفِّس عن معسرٍ ، أو يضع عنه)) [ رواه مسلم: ١٥٦٣ ]

**68.** Kutoka kwa Abuu Qatada رضي الله عنه amesema: nimemsikia Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kuta-ka furaha ya kuokolewa na Allah kwa matatizo ya siku ya Kiyama, basi amfariji mwenye uzito, au amsamehe."* [Amepokea Muslim: 1563]

٦٩- **بذل المعروف**: عن جابر بن عبدالله رضي الله عنهما، عن النبي - ﷺ - قال: ((كل معروفٍ صدقةٌ)) [رواه البخاري ومسلم: ٦٠٢١، ١٠٠٥]

**69. Kutenda mema:** Kutoka kwa Jabir bin Abdillahi رضي الله عنهما kutoka kwa Mtume ﷺ amese-ma, *"Kila jambo jema ni sadaka."* [Amepokea Bukhary na Muslim: 6021, 1005]

٧٠-**السعي على الأرملة والمسكين**: عن أبي هريرة - رضي الله عنه - قال: قال النبي ﷺ: ((الساعي على الأرملة والمسكين كالمجاهد في سبيل الله، أو القائم الليل الصائم النهار)) [متفق عليه: ٥٣٥٣، ٢٩٨٣]

**70. Kuwasaidia wajane na maskini:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kwenda kumsaidia Mjane na (kumsaidia) Maskini, ni sawa na mtu aliyepi-gana Jihadi katika njia ya Allah, au (kama) aliyesimama usiku na akafunga mcha-na."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 5353, 2983]

٧١- **الصدقة**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ : (( من تصدق بِعِدل تمرة من كسب طيب ، و لا يصعد إلى الله إلا الطيبُ ، فإن الله يتقبلها بيمينه، ثم يربِّيها لصاحبه كما يربِّي أحدكم فُلُوَّه حتى تكون مثلَ الجبل )) [ متفق عليه: ٧٤٣٠، ١٠١٤]

**71. Sadaka:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema, *"Atakayetoa Sadaka kiasi cha Tende moja tu, kutokana na chumo la halali, na hayapandi (kwenda) kwa Allah, isipokuwa mambo mazuri, Hakika Allah Ataipokea hiyo sadaka kwa Mkono Wake wa Kuume, kisha Atailea hiyo kwa ajili ya yule aliyeitoa, kama anavyolea mmoja wenu mtoto wa Ngamia wake mpaka itakuwa kama Mlima."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 7430, 1014]

٧٢- **الدعاء للمسلمين**: عن أبي الدرداء ـ رضي الله عنه ـ قال: كان رسول الله ـ ﷺ ـ يقول: (( دعوة المرء المسلم لأخيه ـ بظهر الغيب ـ مستجابة ، عند رأسه مَلَكٌ موَكَّل ، كلما دعا لأخيه بخير ، قال المَلَكُ الموكل به: آمين ، ولك بمثل )) [ رواه مسلم: ٢٧٣٣ ]

**72. Kuwaombea Dua Waislam:** Kutoka kwa Abuu Dar-daa رضي الله عنه amesema: alikuwa Mtume ﷺ akisema, *"Dua ya Muislam kumuombea ndu-*

*gu yake kwa siri, ni yenye kujibiwa, kichwani kwake kuna Malaika aliyewakilishwa, kila anapomuombea ndugu yake jambo la kheri, anasema: 'Amiin nawe upate mfano wake.'"* [Amepokea Muslim: 2733]

٧٣- **صلة الرحم**: عن أنس بن مالك ـ رضي الله عنه ـ قال: سمعت رسول الله ـ صلى الله عليه وسلم ـ يقول: (( من سَره أن يُبسط عليه رزقه ، أو يُنْسَأ في أثره ، فليصل رحمه ))

[متفق عليه: ٢٠٦٧ ، ٢٥٥٧ ]

**73- Kuunga undugu:** Kutoka kwa Anas Bin Maliki رضي الله عنه amesema: nimemsikia Mtume صلى الله عليه وسلم amesema, *"Mwenye furaha ya kutaka kukunjuliwa rizki yake, au kuzidishiwa umri wake, basi na aunge udugu wake."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 2067, 2557]

٧٤- **الاحتساب في النفقة على الأهل**: عن أبي مسعود الأنصاري رضي الله عنه ، عن النبي ـ صلى الله عليه وسلم ـ قال: (( إذا أنفق المسلم نفقةً على أهله وهو يحتسبها كانت له صدقة )) [ متفق عليه: ٥٣٥١، ١٠٠٢]

**74. Kutaraji kulipwa wema kwa huduma za familia:** Kutoka kwa Abuu Masoud al-Answary رضي الله عنه kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وسلم amesema, *"Mtu atakapoihudumia familia yake, ilihali*

*anataraji kulipwa kheri kwa hicho, kwake huhesabiwa ni sadaka."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 5351, 1002]

٧٥- **تربية البنات**: عن أنس بن مالك - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله ﷺ: (( من عال جاريتين حتى تبلغا ، جاء يوم القيامة أنا وهو )) وضم أصابعه. [ رواه مسلم: ٢٦٣١]

**75. Malezi ya watoto wa kike:** Kutoka kwa Anasi bin Maliki رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, *"Mwenye kuwalea mabinti wawili mpaka wakabaleghe, atakuja siku ya Kiyama (tukiwa) mimi na yeye."* Akavikusanya vidole vyake. [Amepokea Muslim: 2631]

٧٦- **الصدقة الجارية**: عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله - ﷺ - قال: ((إذا مات الإنسان انقطع عمله إلا من ثلاث: إلا من صدقة جارية ، أو علم ينتفع به ، أو ولد صالح يدعو له ))[رواه مسلم: ١٦٣١]

**76. Sadaka yenye kuendelea:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه Hakika Mtume ﷺ amesema, *"Anapokufa mwanadamu matendo yake yote hukatika, isipokuwa kupitia mambo matatu: Sadaka yenye kuendelea, Elimu yenye*

*manufaa, au Mtoto mwema atayemuombea."* [Amepokea Muslim: 1631]

٧٧- **إماطة الأذى عن الطريق**: عن أبي هريرة ﷺ، عن النبي - ﷺ - قال: ((بينما رجل يمشي بطريق، وجد غصن شوك على الطريق، فأخذه، فشكر الله له ، فغفر له ))[ متفق عليه: ٦٥٢، ١٩١٤ ]

**77. Kuondosha Maudhi njiani:** Kutoka kwa Abuu Hurayra ﷺ kuwa amesema, Mtume ﷺ amesema, "*Wakati mtu anapotembea njiani, akaona tawi lenye miba, kisha akalitoa, basi Allah Anamkubalia tendo lake hilo, na Anamsamehe."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 652, 1914]

٧٨- **الصحة والفراغ**: عن ابن عباس - ﷺ - قال: قال رسول الله ﷺ: (( نعمتان مغبون فيهما كثير من الناس: الصحة والفراغ ))[ رواه البخاري: ٦٤١٢ ].

**78. Afya na nafasi:** Kutoka kwa Ibn Abasi - ﷺ amesema: Mtume ﷺ amesema, "*Nee-ma mbili watu wengi wamenyimwa faida zake: Afya na Nafasi."* [Amepokea Bukhary: 6412]

٧٩- **أجر الصبر على فقد الولد**: عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله - صلى الله عليه وسلم - قال: (( يقول الله تعالى : ما لعبدي المؤمن عندي جزاءٌ إذا قبضت صفِيَّه من أهل الدنيا ، ثم احتسبه إلا الجنة ))[ رواه البخاري: ٦٤٢٤ ]

**79. Malipo ya kusubiri kutokana na kufiwa na mtoto:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه Hakika Mtume صلى الله عليه وسلم amesema, "*Anasema Allah Mtukufu: Hana malipo mja wangu muumini, Nikimchukulia kipenzi chake, katika watu wa duniani, kisha akataraji kheri, isipokuwa pepo"* [Amepokea Bukhary: 6424]

٨٠- **سبعة يظلهم الله في ظله**: عن أبي هريرة رضي الله عنه ، عن النبي - صلى الله عليه وسلم - قال: ((سبعة يظلهم الله - تعالى - في ظله يوم لا ظل إلا ظله: إمام عدلٌ ، وشاب نشأ في عبادة الله ، ورجل قلبه معلق في المساجد ، ورجلان تحابا في الله ، اجتمعا عليه وتفرقا عليه ، ورجل دعته امرأة ذات منصب وجمال ، فقال: إني أخاف الله ، ورجل تصدق بصدقة فأخفاها حتى لا تعلم شماله ما تنفق يمينه ، ورجل ذكر الله خاليًا ففاضت عيناه )) [ متفق عليه: ١٤٢٣، ١٠٣١ ]

**80. Watu saba watakaopata kivuli cha Allah:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وسلم amesema, "*Watu saba, watafuni-kwa na Allah - Mtukufu - katika Kivuli Chake, si-ku ambayo haina kivuli isipokuwa*

*Kivuli Chake: Imam mwadilifu, na Kijana aliyeleleka katika Ibada ya Allah, na Mtu ambaye moyo wake umetundikwa Misikitini, na Watu wawili walio-pendana kwa ajili ya Allah, walikaa pamoja na kutengana kwa ajili Yake, na Mwanaume aliyei-twa na mwanamke mzuri mwenye cheo (ili wakafanye machafu), yeye akasema: 'Mimi ninamuogopa Allah', na Mtu aliyetoa sadaka kwa siri, mpaka mkono wake wa kushoto haukujua kilichotolewa na mkono wa kulia, na Mtu aliyemkumbuka Allah akiwa faragha, kisha akatokwa na machozi."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 1423, 1031]

٨١-**الزيارة في الله** : عن أبي هريرة ﵁ ، عن النبي ﷺ : (( أن رجلاً زار أخاً له في قرية أخرى ، فأرصد الله له على مدرجته ملكًا ( **أي: أقعده على الطريق يرقبه** ) فلما أتى عليه قال: أين تريد؟ قال: أريد أخاً لي في هذه القرية. قال: هل لك عليه من نعمة تربها؟ قال: لا ، غير أني أحببته في الله عز وجل ، قال: فإني رسول الله إليك، بأن الله قد أحبك كما أحببته فيه )). [ رواه مسلم: ٢٥٦٧ ]

**81- Kutembeleana kwa ajili ya Allah**: Kutoka kwa Abuu Hurayra ﵁ kutoka kwa Mtume ﷺ amesema, *"Hakika mtu mmoja alimtembelea ndugu yake katika kijiji kingine, Allah Alimuwekea*

*Malaika njiani (akimsubiri), alipomfikia akamuuliza: 'Wapi unakusudia kuenda?' Akasema: 'Namkusudia ndugu yangu kwenye hiki kijiji.' Akamuuliza: 'Kuna neema yeyote unaitaraji kutoka kwake?' Akasema: 'Hapana! Isipokuwa mimi ninampenda kwa ajili ya Allah.' Akasema: 'Hakika mimi ni Mjumbe wa Allah kwako, ya kwamba Allah Amekupenda kama ulivyompenda kwa ajili Yake."* [Amepokea Muslim: 2567]

٨٢- **البعد عن يسير الشرك**: عن جابر بن عبدالله - رضي الله عنه - قال: سمعت رسول الله - صلى الله عليه وسلم - يقول: (( من لقي الله لا يُشرك به شيئًا دخل الجنة، ومن لقيه يُشرك به شيئًا دخل النار )) [رواه مسلم:٩٣]

**82. Kujiweka mbali na Shirki chache:** Kutoka kwa Jabir bin Abdallah رضي الله عنه amesema: nimemsikia Mtume صلى الله عليه وسلم amesema, "*Yeyote atakayekutana na Allah, akawa hajamshirikisha na chochote, ata-ingia peponi, na atakayekutana na Allah akawa amemshirikisha, ataingia motoni."* [Amepokea Musli-m: 93]

٨٣- **السنة الحسنة**: عن جرير بن عبدالله - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: ((من سن في الإسلام سُنةً حسنةً، فله أجرها، وأجر من عمل بها بعده، من غير أن ينقص من أجورهم شيءٌ، ومن سن في الإسلام سنةً سيئةً،

كان عليه وزرها ووزر من عمل بها من بعده ، من غير أن ينقص من أوزارهم شيءٌ ))[ رواه مسلم: ١٠١٧ ]

**83. Sunna nzuri:** Kutoka kwa Jarir bin Abda-llah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, "*Atakayeanzisha katika Uislam Sunna (mwenendo) nzuri, atapata malipo ya hilo jambo, na malipo ya waliotenda baada yake, bila kupungua chochote kwenye malipo yao, na atakayeanzi-sha katika Uislam Sunna mbaya, atapata madhambi ya hilo, na (atapata) madhambi ya watakaofanya baada yake, bila kupungua cho-chote katika madhambi yao.*" [Amepokea Muslim: 1017]

٨٤– **قتل الوزغ**: عن أبي هريرة ـ رضي الله عنه ـ قال: قال رسول الله ﷺ : (( من قتل وَزَغًا في أول ضربة كتبت له مئة حسنة ، وفي الثانية دون ذلك ، وفي الثالثة دون ذلك )) [ رواه مسلم: ٢٢٤٠ ]

**84. Kuua mjusi:** Kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema, "*Atakayemuua Mjusi katika pigo la kwanza, ataandikiwa mema mia moja, na akiua kwa pigo la pili, (ataandikiwa) chini yake, na akiua kwa pigo la tatu (ataandikiwa) chini yake.*" [Amepokea Muslim: 2240]

٨٥- **المداومة على العمل الصالح وإن قلّ**: عن عائشة رضي الله عنها، أنها قالت: سُئل رسول الله ﷺ: أي الأعمال أحب إلى الله؟ قال: (( أدوَمُها وإن قلَّ ))
[متفق عليه: ٦٤٦٥، ٧٨٢]

**85. Kudumu na matendo mema, japo ni machache:** Kutoka kwa Aisha رضي الله عنها Hakika yeye amesema: Aliulizwa Mtume ﷺ, "Ni mate-ndo gani yanapendeza zaidi kwa Allah?" Akase-ma: *"Yale yanayodumishwa, japo ni macha-che."* [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 6465, 782]

***Shukrani zote ni Zake Allah Ambae kwa Neema Zake ndio hutimia mambo mema.***

# Yaliyomo:

1. Utangulizi ........................................................ 3
3. Fadhila za Qur'an Tukufu ...................................... 5
4. Suratu *al-Ikhlas* ................................................ 6
5. Sura mbili za kinga .............................................. 7
6. Sura *al-Baqarah*.................................................. 7
7. Suratu *al-Baqara* na *Ali Imraan* ............................... 8
8. Aayatu *al-Kursiy* ................................................. 9
9. Mwisho wa Surat *al-Baqarah* .................................. 9
10. Kuhifadhi mwanzo wa *Surat Al-Kahfi*.................. 10
**Fadhila za Kumtaja Allah Mtukufu**..................... 11
11. Kumtaja Allah Mtukufu kwa wingi ...................... 11
12. Na kutoka kwa Abuu Mussa ............................... 11
13. Kumsabihi Allah ................................................ 12
14. Hakuna Hila wala uwezo isipokuwa kwa Allah..... 16
15. Bwana wa Msamaha........................................... 16
16. Dua wakati unapoamka usiku Usingizini............. 17
17. Kutamka neno (*Laa ila-ha illa Allah*)................... 18
18. Ubora wa Vikao ya Kumtaja Allah........................ 20
19. Kumswalia Mtume ............................................. 20
20. Kumshukuru Allah baada ya kula na kunywa ...... 21
**Fadhila za Udhu na Swala** .................................. 22
21. Kutawadha vizuri ............................................... 22
22. Shahada baada ya Udhu..................................... 23

23. Kumfatisha anayeadhini kisha kumsalia Mtume.. 23
24. Dua baada ya kusikia Adhana ........................... 24
25. Fadhila ya Adhana ............................................ 24
26. Kujenga Misikiti ............................................... 25
27. Kuitikia Amiin pamoja na Imam.......................... 26
28. Kuwahi Swala mapema ...................................... 26
29. Kujitwaharisha nyumbani kwenda Msikitini.. ....... 27
30. Hatua nyingi kwenda Misikitini .......................... 27
31. Kudumisha Sunna za *Rawatib* ............................ 28
32. Kisimamo cha usiku ........................................... 29
33. Kuswali Jamaa, Ishaa na al-Fajiri ........................ 29
34. Kuhudhuria Swala ya Ijumaa............................... 30
35. Kuwahi mapema katika Swala ya Ijumaa ............ 30
36. Kuswalia maiti na kushuhudia mazishi yake ........ 31
**Fadhila za Swaumu** ............................................. 32
37. Kufunga Ramadhani kwa kumuamini Allah.......... 32
38. Kusimama Usiku wa Ramadhani......................... 32
39. Kufunga siku sita za *Shawwal* (Mfungo mosi) ..... 33
40. Kufunga siku tatu kila mwezi.............................. 33
41. Kufunga siku ya Arafa ...................................... 34
42. Kufunga siku ya Aashuraa ................................. 34
**Fadhila Mbali Mbali** ............................................. 35
43. Toba (Kutubia) .................................................. 35
44. Fadhila ya Hijja na Umra ................................... 35
45. Kutenda mema mengi Siku 10 za Mfungo 3 ....... 36
46. Kutafuta Elimu ................................................... 36
47. Kujifunza Dini .................................................... 37

48. Kuwalingania watu kwa Allah .............................. 37
49. Kuamrisha mema na kukataza maovu................. 38
50. Kusalimiana ...................................................... 38
51. Kupenda kwa ajili ya Allah.................................. 38
52. Kusema ukweli .................................................. 39
53. Tabia njema ...................................................... 39
54. Bashasha ya uso................................................. 40
55. Kumtembelea Mgonjwa ...................................... 40
56. Upole ............................................................... 41
57. Subira .............................................................. 41
58. Kulea mtoto yatima ........................................... 42
59. Kutatua shida za watu ....................................... 42
60. Kutoka kwa Abuu Qatada .................................. 43
61. Kutenda mema .................................................. 43
62. Kuwasaidia wajane na maskini ........................... 43
63. Sadaka.............................................................. 44
64. Kuwaombea Dua Waislam.................................. 44
65. Kuunga undugu ................................................. 45
66. Kutaraji kulipwa wema kwa hutuma za familia.... 45
67. Malezi ya watoto wa kike.................................... 46
68. Sadaka yenye kuendelea .................................... 46
69. Kuondosha Maudhi njiani ................................... 47
70. Afya na nafasi.................................................... 47
71. Malipo ya kusubiri kwa kufiwa mtoto..................48
72. Watu saba watakaopata Kivuli cha Allah ............ 48
73. Kutembeleana kwa ajili ya Allah ......................... 49
74. Kujiweka mbali na Shirki chache ........................ 50

75. Sunna nzuri ........................................................51
76. Kuua mjusi ........................................................51
77. Kudumu na matendo mema, japo ni machache ..52